



Maelezo juu ya dawa



Nevirapine (Viramune)

Kwa Nini Nimepewa Dawa Ya Nevirapine?

- Nevirapine (inayojulikana pia kama Viramune) ni dawa inayotumika pamoja na mchanganyiko wa dawa nyingine kutibu maambukizi ya vijidudu vya ukimwi.
- Nevirapine husaidia kuzuia protini inayoitwa "reverse transcriptase." Kutokana na kazi hii, dawa hii huwekwa kwenye kundi la dawa zinazoitwa Reverse Transcriptase Inhibitors (RTIs). Vijidudu vya maambukizi ya ukimwi huhitaji protini hii ili kuzaliana, kwa hiyo kwa kuwa dawa hii huzuia protini hii inasaidia kupunguza nguvu za ugonjwa wa maambukizi ya vijidudu vya ukimwi.
- Matumizi ya dawa hii huweza kupunguza wingi wa vijidudu vya maambukizi mwilini mwako. Pia husaidia kupunguza uwezekano wa kupatwa na magonjwa yanayoendana na ukimwi, na kukuwezesha kuwa na afya njema kwa muda mrefu au kukurudishia afya yako kabisa. Vilevile dawa hii husaidia kupunguza uharibifu wa mfumo wako wa kupigana na magonjwa.

Nitatumiaje Dawa Hii?

- Nevirapine hupatikana kwenye vidonge vyenye miligramu 200. Matumizi ya kawaida ya Nevirapine ni miligramu 200 (kidonge kimoja) mara moja kwa siku kwa wiki mbili za mwanzo, kisha huongezwa kuwa miligramu 200 mara mbili kwa siku. Utumiaji huu husaidia kupunguza madhara yaletwayo na matumizi ya nevirapine.
- Nevirapine inaweza kutumika kabla au baada ya chakula.
- Nevirapine inahitajika kuhifadhiwa kwenye joto la kawaida na mahali pakavu.
- Hifadhi dawa hii mbali na watoto.



Canadian AIDS Treatment
Information Exchange
Réseau canadien
d'info-traitements sida

www.catie.ca



www.apaa.ca

Decisions about particular medical treatments should always be made in consultation with a qualified medical practitioner knowledgeable about HIV-related illness and the treatments in question.

Nifanye Nini Nikisahau Kunywa Vidonge Vyangu?

- Meza dawa zako ulizosahau mapema iwezekanavyo. Ikiwa ni karibu na saa mbili kabla ya muda wa kumeza dawa nyingine, endelea na ratiba yako ya kawaida. Usimeze dawa zako mara mbili ya kiwango utakiwacho ili kulipizia ile uliyosahau.
- Tafiti za kisanyansi zilizofanyika karibuni zimegundua kuwa ili dawa za kupigana na maambukizi ya vijidudu vya ukimwi ziweze kufanya kazi vizuri, dawa zote hazina budi kutumiwa mara kwa mara na kwa mfululuzo ilivyoelekezwa. Kuacha au kuruka kumeza dawa zako kunasababisha kupungua kwa nguvu za dawa hizi na kuvifanya vijidudu vya maambukizi kubadilika na kuwa sugu kwa dawa.

Madhara Ya Yaletwayo Na Matumizi Nevirapine Ni Yepi?

- Adhari kuu itokanayo na matumizi ya nevirapine ni upele mdogomdogo unaoshambulia kwenye ngozi, ambao hujitokeza wiki sita za mwanzo za matumizi ya dawa hii. Kama upele huu utajitokeza wiki mbili za mwanzo baada ya kuanza kutumia nevirapine, usiongeze kiwango cha matumizi ya dawa hii hadi utakapoonana na daktari au mfamasia wako.
- Kama upele huu si wa kutisha, kwa kawaida huweza kutibiwa kwa kutumia dawa za kawaida za upele na mwili wako huweza kuzoea dawa hii baada ya muda.
- Kama hali ya upele huu wa ngozini ni ya kutisha — pamoja na dalili za homa, vidonda vya mdomoni, maumivu ya mishipa na maungo ya mwili, kuvimba kwa jicho au macho kuwa mekundu — sitisha matumizi ya dawa hii na wasiliana na daktari au mfamasia wako mara moja.
- Madhara mengine yatokanayo na matumizi ya dawa hii ni kama:
 - Maumivu ya kichwa
 - Kuvurugikwa kwa tumbo
 - Kuhara
 - Homa
 - Uchovu wa mwili wa mara kwa mara
- Adhari nyingine ndogo itokanayo na matumizi ya nevirapine ni kama hepatitis (kuvimba kwa ini), ambako hutokea kwa asilimia 1 (1%) ya watu wanaotumia na kuweza sababisha madhara makubwa kama kusipotibiwa mapema.

Wasiliana na daktari wako au mfamasia kama una dalili za madhara haya. Usisitise au kubadilisha kiwango chako cha matumizi ya dawa hii kabla ya kuongea nao. Wao



Nevirapine (Viramune)

wanaweza kuwa na mawazo mazuri ya jinsi gani ya kubiliana na madhara hayo bila kusitisha dawa hii.

Je, Naweza Kutumia Nevirapine Na Dawa Nyingine?

- Nevirapine inaweza kuleta madhara kadhaa ikitumiwa pamoja na dawa nyingine. Ni muhimu kumweleza daktari wako au mfamasia wako juu ya dawa nyingine zote ulizoandikiwa na unazotumia, (ikiwa ni pamoja na vitamini na dawa za mitishamba).
- Kama unatumia nevirapine, epukana na kutumia dawa ya Rifampin.
- Nevirapine huweza punguza viwango vya damu kwenye methadone na dawa nyingine za kupigana na vijidudu vya maambukizi ya ukimwi zilitwazo protease inhibitors:
 - saquinavir (Fortovase and Invirase)
 - indinavir (Crixivan)
 - ritonavir (Norvir)
 - nelfinavir (Viracept)
 - lopinavir (Kaletra)
 - amprenavir (Agenerase)

Kama unatumia nevirapine na dawa yeyote kati ya zilizotajwa hapo juu, viwango vyake matumizi vitahitajika kubadilishwa.

- Nevirapine huweza punguza utendaji na nguvu za dawa za uzazi wa majira. Kama unatumia nevirapine, itakubidi kutumia njia nyingine ya uzazi wa majira.

Je Naweza Kutumia Nevirapine Na Pombe Au Dawa Za Mitaani?

- Kwa ujumla inashauriwa kuepukana na unywaji mzito wa pombe na dawa za mitaani unapotumia dawa za kupigana na maambukizi ya vijidudu vya ukimwi.
- Pombe huweza kuingiliana kiutendaji na baadhi ya dawa zako. Usiruke au kuacha kutumia dawa zako kama ulivyoelekezwa kwa kuwa unataka kunywa pombe.

Je, Naweza Kutumia Nevirapine Kama Ni Mjamzito Au Nanyonyesha?

- Kama u mjamzito na unataka kutumia Nevirapine, tafadhali pata ushauri kutoka kwa daktari wako.
- Kwa kuwa vijidudu vya maambukizi ya ukimwi huweza kuambukizwa kwa kunyonyesha, wanawake wenye mambukizi ya vijidudu vya ukimwi hawashauriwi kunyonyesha.



Nevirapine (Viramune)

Natakiwa Kujihadhari Vipi Zaidi Ninapotumia Nevirapine?

- Nevirapine inaweza kuadhiri ini lako, na mara chache huweza sababisha aina fulani ya kuvimba kwa ini - hepatitis. Timiza mihadi na daktari wako kwa ajili ya kutazamwa ini lako kama linafanya kazi vizuri.
- Hakikisha una dawa za kutosha kuendelea na matibabu yako.
- Nevirapine haiui vijidudu vya maambukizi ya ukimwi au kutibu ukimwi. Pia haizui kusambaa au kuambukiza kwa vijidudu vya maambukizi ya ukimwi, hivyo tafadhali jaribu kuwa mwangalifu na kutumia kinga zihitajikazo unapotaka kukutana kimwili na mtu mwingine (tumia kondom) au kama unatumia madwa ya kulevya (tumia mabomba na sindano mpya na safi).

Disclaimer: The Canadian AIDS Treatment Information Exchange (CATIE) and Africans in Partnership Against AIDS (APAA) in good faith provide information resources to help people living with HIV/AIDS who wish to manage their own health care in partnership with their care providers. Information accessed through or published or provided by CATIE or APAA, however, is not to be considered medical advice. We do not recommend or advocate particular treatments and we urge users to consult as broad a range of sources as possible. We strongly urge users to consult with a qualified medical practitioner prior to undertaking any decision, use or action of a medical nature.

We do not guarantee the accuracy or completeness of any information accessed through or published or provided by CATIE or APAA. Users relying on this information do so entirely at their own risk. Neither CATIE, nor APAA, nor Health Canada, nor any of their employees, directors, officers or volunteers may be held liable for damages of any kind that may result from the use or misuse of any such information. The views expressed herein or in any article or publication accessed or published or provided by CATIE or APAA are solely those of the authors and do not reflect the policies or opinions of CATIE or APAA, or the official policy of the Minister of Health Canada.

Copyright: This Fact Sheet is made available through a collaboration between Africans in Partnership Against AIDS (APAA), Asian Community AIDS Services (ACAS) and the Canadian AIDS Treatment Information Exchange (CATIE). Original content developed by ACAS, 2001. Translation into Swahili and Hausa by APAA, 2004.

This information is also available in Chinese, Tagalog and Vietnamese

Funding has been provided by Health Canada, under the Canadian Strategy on HIV/AIDS

Supported by an unrestricted educational grant from GlaxoSmithKline in partnership with Shire BioChem



partnership
in partnership with

